Swahili

# Mpango wa Kitaifa wa Bima ya Walemavu na Haki za Washiriki

Mpango wa Kitaifa wa Bima ya Walemavu (NDIS) ni njia mpya ya watu wenye ulemavu kupata usaidizi wanaohitaji ili kuishi maisha mazuri.

## NDIS na haki zako za:

- Kuwa salama, kuheshimiwa na kupata usaidizi na huduma bora.
- Kuomba mkalimani mwenye sifa zinazotakiwa ili kukusaidia kuzungumza na watoa huduma wote, hii inamaanisha NDIA na huduma zinazokusaidia kama sehemu ya Mpango wako wa NDIS.
- Kuchagua huduma unazopokea na jinsi zinavyotoa usaidizi kwako.
- Kuzungumzia wasiwasi wako na uwasilishe malalamiko ikiwa hujafurahishwa na uamuzi au huduma unazopokea.

## NDIS inaamua:

- Ikiwa unaweza kupata usaidizi kutoka kwa NDIS
- Aina ya usaidizi ambao unaweza kupata
- Kiwango cha usaidizi ambacho unaweza kupata

## Ikiwa hujafurahishwa na uamuzi wa NDIA unaweza:

1. Kuomba NDIA kukagua uamuzi huu, ukaguzi huu unaitwa ukaguzi wa ndani. Una miezi 3 kutoka wakati unapokea mpango wako au barua ya uamuzi kuomba NDIA kupitia tena uamuzi.

2. Ikiwa hujafurahishwa na matokeo ya ukaguzi wa ndani unaweza kuomba uamuzi upitiwe tena na **Jopo la Rufaa la Wasimamizi**, ukaguzi huu unaitwa **ukaguzi wa nje.**

3. Unaweza kupata usaidizi wa kuomba ukaguzi wa nje kutoka kwa **Maafisa wa Kusaidia Kuwasilisha Maombi ya Rufaa wa NDIS** ambao si sehemu ya NDIS. (Angalia ukurasa unaofuata kwa orodha ya mashirika ya Rufaa ya NDIS katika Queensland).

## Jinsi ya kupata usaidizi wa kutekeleza Mpango wako wa NDIS

Ikiwa unahitaji kusaidiwa ili kupata usaidizi na huduma ambazo ni sehemu ya Mpango wako wa NDIS, unaweza kuwasiliana na:

- Mratibu wako wa usaidizi, ikiwa unapokea usaidizi huu katika Mpango wako wa NDIS
- Mratibu wa ndani (LAC) katika eneo lako: https://www.ndis.gov.au/contact/locations
- Ofisi ya NDIS iliyo katika eneo lako: Piga simu kwa 1800 800 110 na uombe kuzungumza na ofisi ya NDIS ya eneo lako.



(07) 3354 4900
info@amparo.org.au
53 Prospect Rd, Gaythorne 4051
PO Box 2065, Brookside Centre 4053
www.amparo.org.au

AMPARO Advocacy inc

# Ni SAWA kuzungumzia suala lolote na ni SAWA kuwasilisha malalamiko

1. Una haki ya kuzungumza kuhusu wasiwasi wako na kutoa malalamiko kuhusu NDIA, ikiwa hujafurahishwa na huduma zao. Unaweza kufanya hivi kwa:

    - Kuzungumza na mtu aliye katika ofisi ya NDIA
    - Kujaza fomu ya malalamiko na kuipeleka kwenye ofisi ya NDIA
    - kupigia simu NDIA kwa 1800 800 110
    - kutuma barua pepe kwa feedback@ndis.gov.au.
    - Kupiga simu kwa Ofisi ya Jumuiya ya Madola ya Kupokea Malalamiko Dhidi ya Maafisa wa Mahakama: Simu: 1300 362 072
    - Ikiwa hujafurahishwa na matokeo ya hatua hii unaweza kuwasiliana na shirika la kutetea haki la eneo lako (Angalia orodha ya mashirika ya kutetea haki).

2. Unaruhusiwa kuzungumza na kutoa maoni au kuwasilisha malalamiko kuhusu huduma unazopokea kama sehemu ya Mpango wako wa NDIS. Ikiwa hujafurahishwa unaweza:

    - Kuzungumza na mtoa huduma wako kuhusu wasiwasi wako ili ujue ikiwa wanaweza kukusaidia. Wanaweza kuboresha jinsi wanavyokusaidia wewe au mwanafamilia wako. Unaweza pia kumwomba mtu unayemwamini au wakili kukusaidia kuzungumza na mtoa huduma. (Angalia orodha ya mashirika ya kutetea haki).
    - Kubadilisha watoa huduma, hii inamaanisha kuwa unaweza kuchagua huduma mpya au mratibu mpya wa usaidizi. Unaweza kuomba NDIA, Mratibu wa Eneo Lako au wakili ili kukusaidia kufanya hili.
    - Wasiliana na **Tume ya Ubora na Ulinzi wa Haki ya NDIS** na wanaweza kuhakikisha kuwa haki zako zinalindwa na unapokea usaidizi na huduma bora. **Tume** hutoa usaidizi huru, wa bila malipo na wa siri ili kuhakikisha kuwa washiriki wa NDIS wanapata usaidizi unaofaa.

# Mashirika ambayo yanaweza kukusaidia kuwasilisha malalamiko, rufaa na maombi ya ukaguzi.

1. **Tume ya Ubora na Ulinzi wa Haki ya NDIS**

Simu: 1800 035 544 (simu ya bila malipo kwa simu za mezani)
www.ndiscommission.gov.au/participants/complaints
Huduma ya Kutafsiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS National)) Simu: 131 450 National Relay Service https://internet-relay.nrscall.gov.au
Tuma barua kwa S.L.P 210, Penrith, NSW 2750



(07) 3354 4900
info@amparo.org.au
53 Prospect Rd, Gaythorne 4051
PO Box 2065, Brookside Centre 4053
www.amparo.org.au

2. Mashirika ya Kuwasilisha Rufaa ya NDIS katika Queensland

- Speaking Up For You Inc.: Brisbane / Moreton Bay SIMU: 07 3255 1244 au Barua pepe: sufy@sufy.org.au
- Queensland Advocacy Inc. (Shirika la Kutetea Haki za Walemavu la Queensland) : SIMU ya Jimbo zima: 07 3844 4200 au 1300 130 582 au Barua pepe: NDISAppealsSupport.qai@qai.org.au
- People with Disability Australia Inc.: SIMU ya Jimbo zima:02 9370 3100 au 1800 422 015 Barua pepe: pwd@pwd.org.au
- Independent Advocacy in the Tropics: Townsville na maeneo yaliyo karibu SIMU: 1800 887 688 Barua pepe: reception@iat.org.au
- Rights in Action Inc: Cairns, Yarrabah, Tablelands - Atherton and Mareeba SIMU: 07 4031 7377 Barua pepe: info@ rightsinaction.org

3. Mashirika ya kutetea haki katika Queensland

Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuzungumzia wasiwasi wako unaweza kupata usaidizi kutoka kwa mashirika ya kutetea haki kufanya hivyo.

| | |
|---|---|
| AMPARO Advocacy *(Brisbane)* | 3354 4900 |
| Capricorn Citizen Advocacy *(Rockhampton)* | 4922 0299 |
| Gold Coast Disability Advocacy Inc. | 5564 0355 |
| Independent Advocacy in the Tropics *(Townsville)* | 4725 2505 |
| Ipswich Regional Advocacy Service | 32816006 |
| Mackay Advocacy Inc. | 4957 8710 |
| Queensland Advocacy Inc. | 3844 4200 |
| Rights In Action Inc. *(Cairns)* | 4031 7377 |
| Speaking Up For You Inc. *(Brisbane/ Caboolture)* | 3255 1244 |
| Sunshine Coast Citizen Advocacy | 5442 2524 |
| The Advocacy and Support Centre Inc. *(Ipswich)* | 3812 7000 |
| The Advocacy and Support Centre Inc. *(Toowoomba)* | 4616 9700 |
| People with Disability Australia Inc. *(Bundaberg, Fraser Coast, Logan, Mt Isa, Sunshine Coast)* | 1800 422 015 |

4. Ofisi ya Jumuiya ya Madola ya Kupokea Malalamiko Dhidi ya Maafisa wa Mahakama

Ni shirika huru ambalo linaweza kuchunguza malalamiko kuhusu mashirika ya Serikali ya Australia, ikiwa ni pamoja na NDIA. Simu: 1300 362 072 au Huduma ya Ukalimani na Utafsiri (Translating and Interpreting Service) (TIS National) Simu: 131 450 www.ombudsman.gov.au/what-we-do/working-with-people-with-disability


(07) 3354 4900
info@amparo.org.au
53 Prospect Rd, Gaythorne 4051
PO Box 2065, Brookside Centre 4053
www.amparo.org.au